

Maswali

1. Nani alimpa Sulemani hekima na mali?
2. Sulemani alijuaje mama wa mtoto wa kweli?
3. Nani aliyeishi nchi ya mbali na akasikia habari ya hekima ya Sulemani?
4. Malkia wa Sheba aliamini yote aliyambiwa?
5. Malkia wa sheba alimletea Sulemani nini?
6. Sulemani alijibu yale majibu magumu?
7. Malkia wa Sheba alisema nini juu ya utajiri wa Sulemani?

Majibu

1. Mungu alimpa Sulemani hekima na mali.
2. Sulemani aliposema, "Kata mtoto kwa vipande viwili."
3. Malkia wa Sheba ndiye alisikia kuhusu Sulemani.
4. La hasha, hakuamini yote aliyoyasikia.
5. Malkia wa Sheba alimletea Sulemani dhahabu, manukato na vito vyta thamani.
6. Ndiyo, Sulemani alijibu maswali yake yote.
7. Alimwambia kwamba kila kitu alichoambiwa ni ukweli.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

26 Malkia wa Sheba

Marejeo

1 Wafalme 10

Kiini cha somo

Kuonyesha hekima na mali nyingi yenyewe Mungu alimpea Sulemani

Maneno maalum

1. Sulemani + kipawa kutoka kwa Mungu + hekima na utajiri
2. Wanawake wawili + mtoto aibwa + hukumu + kata mara mbili + mama wa kweli.
3. Malkia wa Sheba + hekima ya Sulemani
4. Zuru + zawadi + amini

26.1 Mfalme Daudi alipokufa, Sulemani mwanawe alitawala Israeli kama mfalme. Mwanzo wa utawala, Mungu alitaka aulize ni kipawa gani angempa. Mfalme Sulemani aliogopa sana kuwa mfalme. Kwa hivyo aauliza Mungu ampe hekima ya kutawala Israeli vizuri. Mungu alifurahi na akampa hekima nyingi. Dunia nzima hakukuwa na mtu aliye kuwa na hekima ya kuzidi Sulemani. Tena akamfanya Sulemani kuwa tajiri.

26.2 Siku moja wanawake wawili walikuja kwa Sulemani awaamue.

“Eh! Mfalme,” mwanamke wa kwanza akasema. “Sisi wawili tunaishi katika nyumba moja. Nilizaa mtoto na baada ya siku tatu huyo mwenzangu naye akazaa mtoto. Ni sisi tu tunakaa kwa hiyo nyumba. Mtoto wa huyu mwanamke alikufa kwa sababu alimlalia. Usiku wa manane, nilipokuwa nikilala aliamka na kumchukua mtoto wangu na kuniwekea aliyekufa kando yangu.”

“Hapana,” mwanamke wa pili alisema, “Mtoto aliyehai ni wangu.” Wale wanawake waliendelea kupishana hali Sulemani anawasikiliza. Alipinduka na kumwambia mtumishi wake. “Niletee upanga.” Walilettea Mfalme Sulemani upanga.

“Kata mtoto aliyehai vipande viwili,” Sulemani alisema, “na ukampe mwanamke huyu nusu na mwingine nusu.” Mwanamke aliyekuwa mama wa kweli wa mtoto akamwambia Mfalme, “Eh bwana wangu, usiuwe mtoto, mpe.” Yule mwingine alisema, “Akawte, vipande viwili.”


Sulemani alitabasamu na kumuangalia yule mama wa kweli. Akasema, “Mpe mwanamke wa kwanza, msimue. Yeye ndiye mamake.” Kila mtu alisikia hekima ya Sulemani na wakajua Mungu amemuekimisha. Waliwaambia watu wengine juu ya hekima na utajiri wake mwingi.

26.3 Malkia wa Sheba aliishi mbali sana na Yerusalem, lakini alisikia juu ya Sulemani na vile alikuwa na hekima. Alisikia maajabu ya nyumba ya Sulemani ya kifalme na hekalu kubwa ya Yerusalem.

Malkia wa Sheba alimletea Sulemani manukato, dhahabu na vito vya thamani. Alizibeba kwa ngamia akienda kumuona huko Yerusalem. Hakuamini yote aliyoambiwa kuhusu Sulemani, alitaka kujionea kwa macho yake mwenywewe.

26.4 Malkia wa Sheba alipowasili Yerusalem, alizungumza na Sulemani na kumuuliza maswali mengi magumu. Aliyajibu yote.

Aliona hekalu ya ajabu aliyoijenga. Aliona karamu kuu alizoandaa, na mavazi mazuri yaliyovaliwa hata na watumishi wake. Kwa hivyo akaamini yote aliyoambiwa alipokuwa kwa nchi yake.



“Ni kweli yote niliyosikia nikiwa kwa nchi yangu kuhusu hekima nyingi na mali yako,” Malkia wa Sheba alimwambia. “Lakini sikuamini mpaka nilipokuja nikajionea kwa macho yangu. Hata sikuambiwa nusu yake.”

Malkia wa Sheba alishusha mizigo kutoka kwa ngamia. Akampa Sulemani dhahabu nyingi, manukato ya harufu nzuri na vito vya thamani vizuri. Malkia wa Sheba alimpa Sulemani manukato mengi yenye Yerusalem haitapata siku nyingine. Sulemani alimpa Malkia wa Sheba kila kitu alichotaka. Akaondoka Yerusalem na kurudi nchini mwake.